Wajibu wako la jambo la kufanya iwapo una matatizo na makao yako

Aprili 2010

Problems with your accommodation - Swahili

Makao yaliyotolewa na Ofisi ya Nyumbani (iliyojulikana awali kama makao ya NASS) lazima yawe safi, salama na yanayoweza kuishika.

Makao yako lazima yawe na vifaa vinavyofaa vya usalama dhidi ya moto na yasiwe na unyevunyevu au kuhitaji utengenezaji mwingi.

Kijitabu hiki kinaonyesha haki na wajibu wako, wajibu wa mtoaji makao, la kufanya iwapo una tatizo na jinsi tunavyoweza kukusaidia.

Wajibu wangu ni upi ninapoishi makaoni?

Lazima:

- Uweke makao yako yakiwa safi na utengeneze fanisho au vifaa vyovyote ulivyopewa;
- Tunza makao na maeneo yaliyo karibu. Kwa mfano, kuhakikisha kuwa ngazi ni safi na hakuna vitu vyovyote njiani, nguo au bidhaa zingine.
- Tupa takataka zozote za nyumbani. Hii ni pamoja na kutoa pipa za taka nje kwenye eneo linalofaa;
- Tuma ombi na upate idhini iliyoandikwa kutoka kwa Ofisi ya Nyumbani kukuidhinisha kupata mgeni atakayelala **kabla** ya kuruhusu mtu kuishi nawe.
- Tuma ombi na upate idhini kutoka kwa Ofisi ya Nyumbani kabla ya kutoka kwa makao yako kwa zaidi ya siku 14 (kwa jumla) katika kipindi cha miezi 6. Iwapo hutapokea idhini **hii kabla ya** kuondoka kwa makao yako. Hii inaweza kusababisha kupoteza makao yako;
- **Ripoti matataizo yoyote** ya makao hayo **kwa mkimu wako haraka iwezekanavyo;** na
- Ruhusu mkimu wa makao kuingia ndani ili kutengeneza.

Scottish Refugee Council, 5 Cadogan Square, (170 Blythswood Court), Glasgow G2 7PH Tel: 0141 248 9799, Fax: 0141 243 2499,
www.scottishrefugeecouncil.org.uk
Scottish Refugee Council is a charity registered in Scotland.
Registered Charity: SC008639

Nifanye nini iwapo nina tatizo na makao yangu?

Iwapo una tatizo na makao yako, unapaswa kuripoti hii kwa mkimu wako wa makao kwanza. Mkimu wako anapaswa kukupata maelezo ya kuwasiliana nao ulihamia kwa makao hayo. Iwapo huna maelezo hayo, wasiliana nasi na tunaweza kukusaidia na hili. Tumia **simu yetu ya bure** katika **0800 085 6087**; fahamu kuwa nambari hii inatumika tu kwa simu za nyaya pekee.

Matatizo ambayo **lazima** yaripotiwe ni pamoja na lakini sio haya tu, masuala kama yaliyoonyeshwa kwenye ramani ifuatayo. Mifano hii ni pamoja na muda uliokadiriwa utakaochukua kuzungumzia tatizo hili.

Suala	**Wakati wa Kujibu/kutengeneza**
Hali za kuishi zisizo salama kama vile, umwagikaji wa gesi, kufurika au uharibifu wa moto	Itikia ndani ya masaa 2 ya kuripotiwa
Hali mbaya sana za maisha kama kukosa maj moto, stima au kingora cha moshi hakifanyi kazi	Itikia ndani ya masaa 24 ya kuripotiwa
Mataizo ya dharura ya maisha kama, uzibaji mdogo, utengenezaji wa ungarishaji au dirisha kukwama	Itikia ndani ya masaa 24 ya kuripotiwa. Shida kutatuliwa katika siku 7 za kuripotiwa
Masuala ya kila mara kama vile uharibikaji wa mashine ya kufua, fanicha kutaka kutolewa au utengenezaji wa mambo ya nje unahitajika.	Shida kutatuliwa katika siku 28 za kuripotiwa

Ni muhimu kukumbuka kuwa una haki ya kuishi katika makao safi na salama. Hupaswi kuwa katika hatari yoyote ya mwili kutoka vifaa vilivyowekwa ndani ya nyumba hiyo, au kutoka kwa majirani au watu wengine.

Iwapo mkimu wa makao yako hatatengeneza shida hyo, tunaweza kuwasiliana nao kwa niaba yako ili kujua mbona tatizo halijatatuliwa au, ikiwezekana, kuwasiliana na Ofisi ya Nyumbani.

Mkimu wa makao yangu anawajibika na nini?

Pamoja na kutoa mahali safi na salama kwako kuishi, mkimu wa makao yako ana wajibu wa:

- Kutoa ‘taarifa ndogo kuhusu mazingira’ unapowasili na katika lugha unayoelewa. Hii ni pamoja na kukuonyesha makao yako, kueleza jinsi ya kutumia vitu na kueleza tondoti za mkataba wako;
- Kutoa kalimani iwapo utahitaji;
- Kukupa tondoti jinsi ya kuwasiliana naye wakati wa dharura;
- Kupanga na kugharamia utengenezaji wa fanicha, vifaa thabiti, mifereji na matatizo yoyote ya mjengo yanayoonekana kuwa hayajatokana na utumiaji vibaya na wewe au wenzi wako.
- Kukueleza kwa maandishi jinsi na lini malalamko yako yatatauliwa. Hii itakuwa thibitisho kuwa umeonyesha shida/lalamiko; na
- Kujibu malalamiko yoyote yanayohusu makao katika muda Fulani. Fahamu kuwa wakati unalingana na uzito wa tatizo na mara nyingine unaweza kuchukua hadi siku 28 kutatua. Rejelea chati katika ukurasa uliopita wa kijitabu hiki kwa mifani.

Nifanye nini iwapo nitapitia,ubaguzi, dhuluma au ushambulizi?

Kwa aina yoyote ya makazi uliyoko, una haki ya kuishi hapo kwa salama, bila woga wa kutishwa au kudhulumiwa. Iwapo mtu anakutendea mabaya kwa sababu ya asili, rangi, tamaduni, jinsi, jinsia au asili ya uraia, ni kosa kubwa sana na ni kinyume cha sheria.

Jambo la kwanza unalopaswa kufanya ni kuwasiliana na polisi wa mtaa ili kuripoti yale ambayo yamekuwa yakitukia; watachunguza tukio hilo. Unaweza kuwasiliana na Polisi ya Strathclyde katika 0141 532 2000 na watafuta mwasiliani wa polisi wa mtaa wako ambaye ataweza kukusaidia kufaili ripoti.

Iwapo unashindwa au huwezi kuongea moja kwa moja na polisi, unaweza kuwasiliana nasi ili tukusaidie katika kuripoti uhalifu huo kwa ufaragha na kama inafaa, tunaweza kukuunganisha na mashirika ambayo yatakusaidia kifikira

Ni muhimu kuwa uweke kumbukumbu ya aina yoyote ya ushambulizi na dhuluma. Unapaswa:

- Kuandika kila kilichotukia, pamoja na muda, tarehe na mahali ambapo kilitukia
- Kuweka barua, arafa, au barua pepe zozote zilizotumwa kwako
- Kuongea na watu wengine (kwa mfano, majirani wengine au wapangaji) ambao wanaweza kuwa waliathiriwa na tabia za mtu huyo.

Scottish Refugee Council is a charity registered in Scotland.
Registered Charity: SC008639